ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 41*** ***18th October, 2024***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.43 Vol. 105 Dated 18th October, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 859 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) ,
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 96 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii imerejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri mpya ifuatayo kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

Sura ya 184

""mifugo" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo;".

Marekebisho ya kanuni ya 7

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 7(4) kwa kuongeza maneno "ndani ya muda usiopungua siku tatu" mara baada ya neno "Halmashauri".

Marekebisho ya kanuni ya 11

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 11(1) kwa kuongeza maneno “bila kufuata kanuni za kilimo” mara baada ya neno “miteremko”.

Marekebisho ya kanuni ya 29

**5**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 29(b) kwa kuongeza maneno “bila sababu ya msingi” mara baada ya maneno “kuzima moto”.

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

**6**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta neno “Wilkanuni” popote lilipotokea na badala yake kuweka neno “Wilaya”.

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*